جنات کا بادشاہ (Swahili)

MFALME WA MAJINI

(na baadhi ya makarama ya Ghaus-e-A'zam رحمۃ اللہ تعالیٰ علیہ)

Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal
MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi دامت برکاتہم العالیہ

جِنَّات کا بَادشاہ

Jinnat ka badshah

MFALME WA MAJINI

na baadhi ya makarama ya Ghaus-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم

Kitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Aĥl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami 'Allāmaĥ Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَة Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wasiliana na Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo. Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf , vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara moja kabla na baada ya dua.

www.dawateislami.net

Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu ii

Mfalme wa Majini 1

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ 1

1. Mfalme wa majini 2

2. Mfuasi wa kweli wa Ghaus-e-A'zam 3

3. Nyoyo zipo kiganjani 5

4. Nisaidie ewe Ghaus-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم 6

Mbinu za Salat-ul-Ghaušiyyaĥ 7

Kuomba msaada kwa asie kuwa Allah عَزَّوَجَلَّ 7

Sayyidunā Issa عَلَيْهِ السَّلَام aliomba msaada kutoka kwa wengine 8

Sayyidunā Musa عَلَيْهِ السَّلَام ameomba msaada kutoka kwa watu 9

Wacha Mungu pia wanasaidia 9

Ansar maana yake ni 'wasaidizi' 10

Mawalii wa Allah عَزَّوَجَلَّ wapo hai 10

Manabii عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام wapo hai 11

Wacha Mungu رَحِمَهُمُ اللّٰهُ تَعَالٰی wapo hai 11

www.dawateislami.net

Imam-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم ameomba msaada kutoka Kwa Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم 12

Imam Būsirī عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان kaomba msaada 12

Kata imeelekea Qiblah 13

Ielekeze kata usawa wa Qiblah..... 14

Kisa cha Yule aliyekuwa na tabia ya kuelekea Qiblah 14

Lulu 13 za madani za kukaa kwa kuelekea Qiblah..... 15

Hadithi tatu za Mtume Mtukufu ﷺ..... 15

Tiba ya Baghdadi 19

Baraka za tiba ya Baghdadi..... 19

Dawa ya Jailani..... 21

www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Mfalme wa Majini

Vyovyote vile shetani atakufanya ujiskie uvivu au uzito, basi kisome kitabu hiki kutoka mwanzo mpaka mwisho اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ imani yako itakuwa nzuri zaidi.

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ

Mtume wa Rahmah صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, Mtetezi wa Umma, wa mwanzo kuingia peponi صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alisema, 'Yeyote atakae nisalia mimi mara mia mbili katika siku ya Ijumaa, atasamehewa madhambi yake ya miaka mia mbili.'

(Jam'-ul-Jawāmi'-lis-Suyuti, juz. 7, uk 199 ., Hadithi 22353)

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

www.dawateislami.net

1. Mfalme wa majini

Abu Saad ‘Abdallah Bin Ahmad alisema, ‘Mara moja, binti yangu Fatimah alitoweka kutoka katika paa la nyumba. Basi nikapatwa na wasiwasi na kwenda kupeleka mashtaka yangu kwa Sultani-ul-Auliya, Sheikh Ghauše-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم na nikamtaka msaada. Akasema, عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِى ‘Nenda Karkh (mji) na kakae nyikani wakati wa usiku na tengeneza upweke uzio wa kiroho (yaani mduara) wewe na nafsi yako tu. Isome بِسْمِ اللّٰه na tafakari juu yangu. Katika nyakati za usiku, misafara mingi ya majini itapita karibu na wewe. Nyuso zitakushtua kwa ugeni uliokuwa wa ajabu sana lakini usitishike. Wakati wa alfajiri, mfalme wa majini atakuja kwako na atakuuliza nini shida yako. Basi utamwambia, ‘Sheikh ‘Abd-ul-Qadir Jilani عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِى amenituma mimi kutoka Baghdadi na nakutaka unitafutie binti yangu aliyepotea.’

Kwa maana hiyo, mimi nikatoka Karkh na nikayafuata maelekezo ya Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم Ndani ya kile kiza cha usiku ule, majini wenye kutisha wakawa wanapita kwenye uzio wangu. Nyuso zao zilikuwa ni za kutisha kiasi kwamba sikuweza kuvumilia kuziangalia. Wakati wa alfajiri, mfalme wa majini alikuja ilhali amepanda farasi pamoja na majini wengine. Alikuwa amebakia nje ya uzio na kuniuliza mimi, ni ipi shida yangu. Mimi nikasema kwamba Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِى alikuwa amenituma kwake. Kusikia vile tu, akashuka farasi na kukaa chini. Majini wengine wakafanya

www.dawateislami.net

hivyo hivyo wakakaa chini ardhini nje ya uzio wangu. Mimi nikampa taarifa kuhusu majanga ya yule binti yangu. Mfalme wa majini akatangaza miongoni mwa majini kwa kuuliza, 'Ni nani aliyemteka nyara msichana?' Muda mfupi tu, jini kutoka china alikamatwa na kuletwa mbele kama mhalifu. Mfalme akamuuliza, 'Kwa nini ukamteka nyara msichana kutoka mji wa Qutb[1] wa zama hizi?' Jini wa Kichina huku akitetemeka alijibu, 'Mtukufu! Mimi nimempenda katika mara yangu ya mwanzo kumuona.' Mfalme aliamuru kichwa cha yule jini wa Kichina kikatwe na binti yangu arejeshwe kwangu.

Kumshukuru Yule mfalme, nikasema, 'Wewe ni mfuasi mkubwa wa Sheikh Ghaus-e-A'zam' Akajibu: 'Wallahi, عَزَّوَجَلَّ wakati Ghaus-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم anapoanza kututazama tu, basi majini wote tunaanza kutetemeka. Na pindi tu Allah عَزَّوَجَلَّ akimteua Qutb, majini wote na wanadamu wanawajibika kumtii yeye.' *(Bahjat-ul-Asrar, uk. 140)*

2. Mfuasi wa kweli wa Ghaus-e-A'zam

Mtu mmoja amesimulia tukio lililotokea katika Kutiyana (Gujarat, India), kijiji cha mababu wa Sag-e-Madīna (mwandishi). Kulikuwa na mtu katika Kutiyana (mji) ambaye alikuwa ana upendo mkubwa sana kwa Ghause-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم. Alikuwa akisherehekea Giyārĥwīn mara kwa mara. Tabia yake

[1] Qutb ni mtu mwenye cheo cha juu kiroho

www.dawateislami.net

nyengine ni kwamba alikuwa akionyesha utiiifu mkubwa na heshima kwa Masayyid. Alikuwa mkarimu sana na mwenye kuwajali sana hata watoto wa masayyid, kiasi kwamba akiwaona tu, anawanunulia pipi tamu.

Alipofariki duniani, kiwiliwili chake kilikuwa kimefunikwa na kitambaa na watu walikuwa wamekaa pembeni mwake kwa huzuni lakini ghafla, yule mfuasi wa kweli wa Ghaus-e-A'zam akainuka na kukaa kitako. Watu wakawa na khofu na waliachwa na mshangao, wakataka kukimbia.

Akawaita na kusema, 'Musiogope, nisikilizeni mimi!' watu walipokuwa karibu nae akasema, 'Nawaambieni ukweli kwamba sasa hivi Murshid[1] wangu, Sheikh 'Abd-ul-Qadir Jilani عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم amenitunukia uwepo wake na ameniambia, 'Mfuasi wangu umefariki bila ya kutubia! Haya inuka upesi utubie.' Roho yangu ikarejea katika kiwiliwili changu ili nije kufanya toba. Baada ya kusema hayo, akaomba msamaha wa madhambi yake na akaitamka kalima.

Hongereni wafuasi wa Ghaus-e-A'zam kwa sababu Sultani wa Baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْهَادِى amesema, 'Mfuasi wangu, hata awe ametenda madhambi kiasi gani, basi hatafariki mpaka afanye toba.' *(Bahjat-ul-Asrar, uk. 191)*

[1] mwongozo wa kiroho

www.dawateislami.net

3. Nyoyo zipo kiganjani

Sheikh Umar Bazar عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان amesema, ‘Ijumaa moja, nilikuwa naelekea katika msikiti pamoja na Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم. Mimi niliwaza moyoni kwamba ni jambo la ajabu kabisa kwamba kawaida ninapoenda msikitini siku ya Ijumaa pamoja na Murshid wangu, watu wengi wanakusanyana karibu yetu na kuanza kumtolea salamu na kumpa yeye mikono hadi inakuwa vigumu sana kuendelea na matembezi yetu; lakini leo hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa na khabari juu yake. Basi baada ya lile wazo kunipitikia ndani ya moyo wangu palepale Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم akaniangalia kwa tabasamu.

Ghafla, watu wakaanza kumkimbilia na kupeana mikono na Sultani wa baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْهَادِى. Kukawa na watu wengi waliosongamana na walituzonga mimi na yeye Murshid wangu عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْهَادِى mpaka mimi nikasema tena moyoni kwamba ilikuwa bora mwanzo. Mara tu wazo hili liliponipitikia moyoni mwangu, yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْه alisema, ‘Ewe Umar! Ilikuwa ni wewe ndie ulie utamani umati wa watu. kwani si unajua kwamba nyoyo za watu zipo katika kiganja changu! Nikitaka nitawafanya wanifuate na nikitaka naweza kuwafanya wasinifuate.’ *(Bahjat-ul-Asrar, uk. 149)*

Kunjiyān dil kī Khuda bali Tujhay din Aisi kar,
Ke Yeh Sina ho mahabbat ka khazanah tayrā

Allah amekupa funguo za nyoyo katika mkono wako
Ufanye moyo wangu uwe hazina ya mapenzi yako

www.dawateislami.net

4. Nisaidie ewe Ghaus-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم

Sheikh Bishr Qarzī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِی amesema, ‘Siku moja nilikuwa (nasafiri) na msafara wa biashara wa ngamia 14 waliobeba sukari. Sote tukakaa katika kambi ndani ya msitu wenye kutisha katika usiku ule. Katika sehemu ya kwanza ya usiku ule, ngamia wetu wane tuliowabebesha sukari wakawa wamepotea. Licha ya juhudi zangu za kuchoka sikuwaona. Msafara ukaondoka na ukaniwacha mimi pamoja na muendesha ngamia wangu.

Asubuhi iliyofuata, mimi nilikumbuka kwamba Murshid wangu, Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم mara moja aliwahi kuniambia, ‘Muda wowote ambao itakukumba shida au tabu liite jina langu, wewe utakuwa ni mwenye kuondokewa na shida uliyonayo.’ Kwa hiyo, mimi nikaanza kuomba msaada nikisema, ‘Ewe Shaykh 'Abd-ul-Qadir! Mimi nimepotelewa na ngamia wangu!’ Hapo hapo akanijia mcha Mungu, akiwa na nguo nyeupe, amesimama juu ya kilima kidogo upande wa mashariki. Yule mcha Mungu akatoa ishara na mimi na muendesha ngamia wangu tukaanza kumfuata na kumsogolea, tulianza kumkaribia akatupotea machoni mwetu. Tukaanza kuangalia kila mahala kwa hali ya mshangao na kuchanganyikiwa kabisa. Ghafla, tukawaona wale ngamia wetu wane wamekaa chini ya bonde. Tukaenda kuwakamata na tukaongoza kwenda kuufuata ule msafara.’

(Bahjat-ul-Asrar, uk. 196)

www.dawateislami.net

Mbinu za Salat-ul-Ghaušiyyaĥ

Wakati Sheikh Abu Al-Hassan Ali Khabbaz عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان alipo simuliwa ule mkasa wa wale ngamia waliopotea, alisema kwamba yeye aliwahi kuambiwa na Sheikh Abu al-Qasim عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان kwamba alimsikia Sheikh 'Abdul-Qadir Jilani عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِی akisema, 'Yule atakae omba msaada wangu katika shida na dhiki basi atapata uokovu wa shida hiyo na atakae nitaja mimi katika muda wa taabu basi atapata nafuu ya taabu hiyo. Yeyote amuombaye Allah عَزَّوَجَلَّ chochote kwa kulitaja jina langu, basi haja yake itatimizwa.'

Mtu atakae sali rakaa mbili za nafli, katika kila rak'at akasoma suratul Ikhlas mara 11 baada ya suratul fatiha na baada ya kutoa salamu amsalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kisha aelekee hatua 11 kwenda Mji Mtukufu wa Baghdad na kuomba shida zake na aombe kutatuliwa haja yake عَزَّوَجَلَّ haja yake itatimizwa.'

(Bahjat-ul-Asrar, uk. 197)

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Kuomba msaada kwa asie kuwa Allah عَزَّوَجَلَّ

Ndugu zangu waislamu! Baada ya kusoma matukio yaliyopita, mtu anaweza kufikiri kwamba ni lazima kuomba msaada kwa Allah عَزَّوَجَلَّ yeye pekee na hakuna mwengine zaidi yake kwa sababu wakati Allah عَزَّوَجَلَّ ana mamlaka ya kutoa msaada, kwa

www.dawateislami.net

nini tuelekee kwa wengine wasio kuwa Allah kwa kuwaomba msaada? Hii ni hatari sana na ni hila ya shetani ambayo huwa anaitumia sana katika kusababisha watu wengi kupotea. Kwa kweli Allah عَزَّوَجَلَّ hajatukataza na kutaka msaada kutoka kwa wengine. Angalia katika Qurani Tukufu ambapo Allah عَزَّوَجَلَّ ameturuhusu katika aya mbalimbali kutaka msaada kutoka kwa wengine. Kwa kweli, licha ya kuwa yeye ni Mwenye nguvu, yeye Mwenyewe عَزَّوَجَلَّ amewahimiza waja wake kuinusuru dini yake; Imeelezwa katika Quran tukufu:

اِنْ تَنْصُرُوا اللّٰهَ يَنْصُرْكُمْ

'kama mutaisaidia dini ya Allah عَزَّوَجَلَّ, pia Yeye عَزَّوَجَلَّ atawasaidia'

(juzuu ya 26, Sura Muhammad, aya 7)

Sayyidunā Issa عَلَيْهِ السَّلَام aliomba msaada kutoka kwa wengine

Sayyidunā Issa عَلَيْهِ السَّلَام aliwataka wafuasi wake msaada. Imeelezwa katika Quran tukufu:

قَالَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ لِلْحَوَارِيّٖنَ

مَنْ اَنْصَارِيْۤ اِلَى اللّٰهِ ؕ قَالَ الْحَوَارِيُّوْنَ نَحْنُ اَنْصَارُ اللّٰهِ

www.dawateislami.net

Nabii Issa alipowaambia wafuasi wake, 'Ni nani wasaidizi wangu kwa (ajili ya kutangaza dini ya) Allah?' wafuasi wakasema sisi ni wasaidizi wa (kutangaza dini ya) Allah.

(juzuu 28, Sura Saf, aya 14)

Sayyidunā Musa عَلَيْهِ السَّلَام ameomba msaada kutoka kwa watu

Wakati Sayyidunā Musa عَلٰى نَبِيِّنَا وَ عَلَيْهِ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام alipotakiwa kwenda kumlingania Firauni, alimuomba Allah عَزَّوَجَلَّ ampatie msaada wa mwanadamu na kumuomba Allah عَزَّوَجَلَّ kama ifuatavyo;

وَ اجْعَلْ لِّيْ وَزِيْرًا مِّنْ اَهْلِيْ ﴿۲۹﴾ هٰرُوْنَ اَخِي ﴿۳۰﴾ اشْدُدْ بِهٖۤ اَزْرِيْ ﴿۳۱﴾

'Na unifanyie waziri katika jamaa zangu, ndugu yangu Haruni (mfanye awe ndie waziri wangu) nitie nguvu kwa (ndugu yangu) huyu' *(Juzuu ya 16, Sura Taha, Aya 29-31)*

Wacha Mungu pia wanasaidia

Allah عَزَّوَجَلَّ amesema mahali pengine:

فَاِنَّ اللّٰهَ هُوَ مَوْلٰىهُ وَ جِبْرِيْلُ

وَ صَالِحُ الْمُؤْمِنِيْنَ ۚ وَ الْمَلٰٓىٕكَةُ بَعْدَ ذٰلِكَ ظَهِيْرٌ ﴿۴﴾

www.dawateislami.net

'Basi kwa hakika Allah ndiye msaidizi wake na Jibril na waislamu wema, na zaidi ya hayo pia Malaika watasaidia.

(Juzuu ya 28, Sura Tahrim, aya 4)

Ansar maana yake ni 'wasaidizi'

Ndugu muislamu, umeshaona? Kwamba Quran imeshatangaza wazi kuwa Allah عَزَّوَجَلَّ ni kweli Msaidizi lakini kwa fadhila zake Allah عَزَّوَجَلَّ, Jibril na watu walio karibu na Allah عَزَّوَجَلَّ (Manabii عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام na watu wema) na hata Malaika wanaweza kusaidia. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Sasa ule wasiwasi wa shetani kwamba hakuna yeyote asiyekuwa Allah عَزَّوَجَلَّ anaeweza kutoa msaada ushaondoka kabisa. La kutia nguvu zaidi ni kwamba watu waliohamia madina wanaitwa Muhajir (masahaba waliohama) na wale walio wasiaidia na kuwaunga mkono ni Ansaar (masahaba waliosaidia) kila mtu aliesoma anaifahamu maana ya neno Ansaar kama ni wasaidizi.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Mawalii wa Allah عَزَّوَجَلَّ wapo hai

Inawezekana kwa Shetani kumfanya mtu afikiri kwamba inaruhusiwa kuomba msaada kutoka kwa mtu hai lakini haijaruhusiwa kwa maiti. Kama utazisoma kwa makini aya zifuatazo na mada inayofuata hapo mbele basi huenda wazo baya la shetani likakutoka kabisa اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Inaelezwa kuwa:

www.dawateislami.net

وَلَا تَقُوْلُوْا لِمَنْ يُّقْتَلُ فِيْ سَبِيْلِ
اللّٰهِ اَمْوَاتٌ ؕ بَلْ اَحْيَآءٌ وَّلٰكِنْ لَّا تَشْعُرُوْنَ ﴿۱۵۴﴾

‘Na wala wala musiseme kuwa wale walio uwawa katika njia ya Allah ni maiti, bali wao ni wahai lakini nyinyi hamtambui’

(Juzuu ya 16, Sura Baqarah, aya 154)

Manabii عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام wapo hai

Kama hii ni sifa ya mashahidi, basi anawezaje mtu kuwa na shaka kuhusu uhai wa Mitume عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام ambao ndio wenye daraja ya juu kuliko mashahidi!

Sheikh Imam Bayhaqi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِی ameandika kitabu chake kuhusu maisha ya Manabii (Hayātul-Anbiya) na ameandika katika Dalāilun-Nubūwwaĥ kwamba Manabii عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام wapo hai kwa Mola wao kama mashahidi.

(Al-Havi lil Fataawa, juz. 2, uk. 263) (Dalāilun-Nubuwwah, juz. 2, uk. 388)

Wacha Mungu رَحِمَهُمُ اللّٰهُ تَعَالٰی wapo hai

Sheikh Shah Walīyullāĥ عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان amesema kuhusu hadhi ya Ghaus-e-A’zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان katika namba 11 ya Ĥam'āt; ‘Yeye ni Sheikh Muhiyyuddīn ‘Abd-ul-Qadir Jilani عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان na yeyé عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان ana uwezo ndani ya kaburi lake kama waliokuwa hai (huku duniani).’ *(Ĥam'at, uk. 61)*

www.dawateislami.net

Hivyo basi, Manabii عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام na watu wema رَحِمَهُمُ اللّٰهُ تَعَالٰی wapo hai na sisi hatuombi msaada kutoka kwa wafu bali tunaomba msaada kutoka kwa wale walioko hai tu. Nasi tunaamini kuwa wao ni wasaidizi kwa idhini yake Allah عَزَّوَجَلَّ na bila ya idhini yake mtume yoyote wala mcha Mungu hawezi kutupatia sisi aina yoyote ile ya msaada.

Imam-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم ameomba msaada kutoka Kwa Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

Imamu wa mamilioni ya wafuasi wa madhehebu ya kihanafi Imam al-A'zam Abu Hanifa رَحْمَةُ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْه Ameomba msaada kwa Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم katika Qasid-e-Un'man:

يَا اَكْرَمَ الثَّقَلَيْنِ يَا كَنْزَ الْوَرٰى جُدْلِیْ بِجُوْدِكَ وَ اَرْضِنِیْ بِرِضَاكَ

اَنَا طَامِعٌ بِالْجُوْدِ مِنْكَ لَمْ يَكُنْ لِاَبِیْ حَنِيْفَةَ فِی الْاَنَامِ سِوَاكَ

Ewe mbora kuliko binadamu wote na majini! Ewe hazina ya Allah عَزَّوَجَلَّ nakuomba unipe kwa ukarimu wako na uniridhishe kwa kuniridhia. Mimi nataraji ukarimu wako. Hakuna msaidizi kwa Abu Hanifa رَحْمَةُ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْه katika watu isipokuwa wewe.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Imam Būsirī عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان kaomba msaada

Sheikh Imam Sharaf-ud-Din Būsirī عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان ameomba

www.dawateislami.net

msaada kutoka kwa Mtume صَلَّی اللّٰہ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم katika kasida yake mashuhuri inayojulikana ‘Qasīdaĥ-e-Burdah’ na akasema: ‘Ewe mbora wa viumbe! Sina mwingine isipokuwa wewe, ambaye atanipatia msaada katika nyakati za shida.

(Qasīṣdaĥ-e-Burdah, uk. 36)

Imdādullāĥ Muhajir Makki عَلَیْہِ رَحْمَۃُ الْمَنَّان ameomba katika kitabu chake cha mashairi chenye jina 'Nālaĥ-e-Imdad:

Laga takyaĥ gunāĥaun Ka para din raat sautā Hun
Mujhay ab Khuwab-e-ghaflat se Jaga do Ya Rasulallah

Nina lala mchana na usiku juu ya mto wa madhambi
Niamshe mimi ewe Rasulallah kutoka katika ndoto za pumbao.

Kata imeelekea Qiblah

Siku moja, kundi la watu wacha Mungu رَحِمَہُمُ اللّٰہُ تَعَالٰی kutoka kijiji cha Jīlān walitembelea mahakama yenye kheri ya Sheikh Ghaus-e-A’zam عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْاَکْرَم na kuona kata (chombo cha kuchukua udhu) yake haikuwa imelekea Qiblah basi wakamfikishia taarifa Ghaus-e-A’zam عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْاَکْرَم juu ya jambo hilo. Yeye رَحْمَۃُ اللّٰہِ تَعَالٰی عَلَیْہ akamuangalia kwa jicho la ghadhabu mtumishi wake ambaye hakuweza kuvumilia hali ya ukali wa Sheikh kwa kuangaliwa kule na akaanguka chini na akatetemeka mpaka akafariki. Kisha Ghaus-e-A’zam عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْاَکْرَم akaitazama kata yake, basi ile kata yenyewe ikaelekea Qiblah. *(Bahjat-ul-Asrar, uk. 101)*

www.dawateislami.net

Ielekeze kata usawa wa Qiblah

Enyi wafuasi wa Sultani wa Baghdadi! Bila shaka, mapenzi ya dhati kabisa ni kufuata kila kitendo cha yule umpendae. Hivyo basi kama inawezekana kuielekeza kata ya kutawadhia upande wa Qiblah basi fanyeni hivyo hivyo. Muhadithi-al- A'zam Maulana wa Pakistani Sheikh Sardar Ahmad رَحْمَةُ اللهِ تَعَالٰی عَلَيْه alikuwa anaielekeza kata yake ya kutawadhia na viatu vyake upande wa Qiblah na mimi Sag-e-Madīnaĥ (mwandishi) huwa nafanya bidii kuzifuata nyayo walizopita wacha Mungu kama hawa (رَحِمَهُمُ اللّٰهُ تَعَالٰی) kwa kuielekeza kata yangu na viatu vyangu upande wa Qibla, bali napenda kila kitu kielekee Qibla.

Kisa cha Yule aliyekuwa na tabia ya kuelekea Qiblah

Ndugu waislamu! Kadri inavyowezekana, tunatakiwa kuendeleza tabia ya kukielekea Qiblah kwa sababu kuna baraka nyingi za kufanya hivyo. Sheikh Imam Burhan-ud-Dīn Ibrahim Zarnūjī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالٰی عَلَيْه anasimulia; ‘Wanafunzi wawili walisafiri nje ya nchi kutafuta utambuzi wa maarifa ya dini. Wote wawili walikuwa katika darasa moja. Wakati waliporudi nyumbani, mmoja wao alikuwa mwanachuoni mkubwa sana na mwengine akabakia kuwa ni mjinga. Wanazuoni wa mji ule wakaanza kufikiria sababu gani iliyowafanya kuwa tofauti. Baada ya kufanyika uchunguzi wa makini katika njia zao za kujifunza, namna zao

www.dawateislami.net

za kudurusu na tabia zao zingine, jambo moja lilionekana wazi kuwa Yule aliyekuwa mwanachuoni alikuwa na tabia ya kulekea Qiblah na Yule mwengine hakuwa na tabia hiyo.

Kwa hivyo basi, wasomi na wanasheria رَحِمَهُمُ اللّٰهُ تَعَالٰی kwa kauli moja wakakubaliana kwamba kwa baraka ya jitihada ya kufuata sunna ya kuelekea Qibla yule mwanafunzi akawa mwanachuoni mkubwa. *(Ta'līm-ul- Muta'allim, uk. 68)*

Lulu 13 za madani za kukaa kwa kuelekea Qiblah

- Mtume Tukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alikuwa na kawaida ya kukaa huku ameelekea Qiblah. *(Ihyā-ul-'Ulūm, juz. 2, uk. 449)*

Hadithi tatu za Mtume Mtukufu ﷺ

- Bora ya vikao vyote ni vile ambavyo watu wake huelekea Qiblah. *(Mu'jam Awsat, juz. 6, uk.161, Hadithi 8361)*

- Kila kitu kina thamani na thamani ya kikao ni kuelekea Qiblah. *(Mu'jam al Kabir, juz. 10, uk320 ., Hadithi 10781)*

- Kila kitu kina utukufu wake na mikusanyiko nayo utukufu wake unapatikana kwa kuelekea Qiblah. *(Mu'jam al Kabir, juz. 2, uk.20, Hadithi 2354)*

www.dawateislami.net

- Ni sunna kwa Muballighīn na walimu kuwa wao wakipe mgongo Qibla ili wasikilizaji (wanafunzi) waweze kukaa ilhali wameelekea Qiblah. Ndio maana, Sheikh Hafidh Sakhāwī رَحْمَۃُ اللّٰہِ تَعَالٰی عَلَیْہ amesema, 'Sababu moja wapo kwamba kwanini Mtume صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alikuwa akikipa mgongo Qiblah, ilikuwa ni kuwaruhusu masahaba waelekee Qiblah.

(Al-Maqasid-ul-hasanah, uk. 88)

- Sayyidunā 'Abdullah Bin Umar رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُمَا mara kwa mara alikuwa anaelekea Qiblah. *(Al Adab al Mufrad, uk 291 , Hadithi 1137)*

- Wakati wa kufundisha Qur'ani Tukufu na elimu, unapaswa kukaa ilhali umekipa mgongo Qiblah kwa niya ya kutekeleza sunnah ili kuwawezesha wanafunzi kuelekea Qiblah. Na wanafunzi wafundishwe sunna, falsafa na nia ya kukaa katika utaratibu huu. Jaribu kukaa ilhali umelekea Qiblah utakapokuwa husomeshi darasani.

- Wanafunzi wanapaswa kuelekea Qibla ikiwa katika kuelekea Qibla wanaweza kumuelekea mwalimu pia (kama haiwezekani basi wamuelekee mwalimu tu) la kama si hivyo itakuwa vigumu kumuelewa mwalimu.

www.dawateislami.net

- Ni sunna kwa Khatib kutoa khutba ilhali amekipa mgongo Qibla ili wale wanaomsikiliza wamuelekee yeye khatib.

- Wakati wa kusoma Qur'an Tukufu, vitabu vya dini, kuandika Fatwa, kutunga kitabu, kuomba dua, kufanya Zikri, kumsalia mtume na wakati wowote ukiwa umekaa chini au umesimama, kama hakunakizuizi chochote kinacho husiana na dini, jaribu kujizoesha tabia ya kuelekea Qiblah kila wakati ili upate thawabu nyingi. (Ikiwa wewe umo ndani ya nyuzi 45 ya Qiblah utakuwa unahisabika kama umeelekea Qiblah).

- Kama inawezekana, weka meza, kiti nk kuelekea usawa wa Qibla ili wakati wowote ukiwa umekaa utakuwa umeelekea Qiblah.

- Kama imekutokea tu ukawa umeelekea Qiblah bila ya kukusudia hivyo basi hutapata ujira wowote. Hivyo basi mtu anatakiwa awe ananuwia nia njema, kwa mfano (1) kupata thawabu ya akhera (2) kutekeleza sunna (3) Ninaelekea Ka'abah kwa heshima yake na utukufu wake. Wakati unajisomea au kufanya utafiti wa vitabu vya Kiislamu na masomo mengine unapaswa kuweka nia kama hizo ikiwa ni pamoja na kwamba kwa kuitekeleza sunnah ya kuelekea Qibla, nitapata baraka ya elimu ya Dini.

www.dawateislami.net

❖ Katika nchi nyingi kama vile, Pakistan, India, Nepal n.k. wakati wowote mtu anapo elekea Qiblah wakati huo huo huwa anakuwa ameelekea Madīnaĥ Munawwarah kwa hivyo basi uongeze nia ya kulekea Madīnaĥ-tul-Munawwarah kwa kuipa heshima.

Baītĥnay Ka Hasin qarīnaĥ nyasi
Rukh Udhar nyasi Jidhar Madīnaĥ nyasi
Dono 'Alam Ka jo nagīnaĥ nyasi
Meray Aqa ka Woh Madīnaĥ nyasi
Ru baru mayray Khana-e-Ka'abah
Aur Afkar kitabu mayn Woh Madīnaĥ

Upande mzuri ulioje kuwa wewe uso
wako ume elekea Madina ambayo
Almasi katika kote kuwili duniani na akhera,
Mji wa Mtume wangu ulio barikiwa, Madina
Mbele yangu na ka'ba ipo ndani ya fikra zangu .

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

www.dawateislami.net

Tiba ya Baghdadi

Usiku wa mwezi 11 wa Rabī'-ul-Ghaus (mwezi 4 ya Kalenda ya Kiislamu), soma majina 11 ya Sheikh Ghaus-e-A'zam عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْاَكْرَم (Soma Salat-'Alan-Nabi mara 11 mwanzo na mwisho wa kuyasema majina hayo) kisha puliza juu ya tende 11 na uzile katika usiku huo huo basi utaipata amani kwa muda wa mwaka mzima, majina yenyewe yapo hapo chini.

1	سَیِّد مُحیُ الدِّیْن سُلْطان	2	مُحیُ الدِّیْن قُطب
3	مُحیُ الدِّیْن خَواجَه	4	مُحیُ الدِّیْن مَخْدُوم
5	مُحیُ الدِّیْن وَلِی	6	مُحیُ الدِّیْن بادشاہ
7	مُحیُ الدِّیْن شَیْخ	8	مُحیُ الدِّیْن مَوْلٰنا
9	مُحیُ الدِّیْن غَوْث	10	مُحیُ الدِّیْن خَلِیْل
11	مُحیُ الدِّیْن		

Baraka za tiba ya Baghdadi

Muhtasari wa ndugu mmoja wa Kiislamu ni kama ifuatavyo: Ijtimai ya Zikri ilifanyika mwezi 11 Rabī'-ul-Ghaus, 1425 AH (2003) katika eneo la Korangi, Babul Madinah Karachi. Wakati wa Bayana ya kuihamasisha sunnah ilipokuwa inafanyika, tiba ya Baghdadi ilitambulishwa. Baada ya Bayana, ilifayika Bay'ah

www.dawateislami.net

ya kujiunga na Silsilah ya Qadiriyya razawiyya. Ghafla nikapatwa na usingizi, basi macho yangu yalipo jifumba, niliona kwamba sheikh Ghaus-e-A'zam عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْاَکْرَم amekaaa na uso wake ni wenye kumemeta na amekitanda kishali chake, nikasogea mbele na nikakishika kwa upande. Na nikahisi kuwa kuna watu wengine pia wamekishikilia lakini sikuweza kumuona yeyote kati yao. Nikayakariri yale maneno yanayosemeshwa wakati wa bay'ah. Hapo hapo baada tu ya ile bay'ah kumalizika, nikapeleka maombi ya kuwa mke wangu ana mimba na anahisi maumivu makali sana. Na daktari ameshauri afanyiwe upasuaji; basi nipatiwe nafuu na janga hili. Akanijibu, 'Tumia tiba ya Baghdadi.' Nikauliza kwa heshima, Ewe Murshid wangu! Muda umeenda na ninatakiwa kuifanya usiku huu huu.' Akanijibu, 'Umeruhusika kuifanya katika mchana, kabla ya siku kumalizika na اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ utabrikiwa watoto mapacha bila ya upasuaji. Wape watoto wako majina ya Hassan na Mushtaq. Wote hao wawili watakuwa chini ya uangalizi wangu.' Nikafanya kama nilivyo amrishwa na nilimpatia mke wangu tende kama inavyotakiwa.

اَلْحَمْدُ لِلّٰہ عَزَّوَجَلَّ! Majibu nikayaona hapohapo na yale maumivu yakapotea kabisa, na mke wangu akajifungua bila ya shoda yoyote ile. Ninashuhudia kuwa nilijaaliwa watoto mapacha wawili kama vile Ghauše-A'zam alivyo ni bashiria, na nikawapa majina ya Hassan na Mushtaq kama ilivyo agizwa.'

www.dawateislami.net

Dawa ya Jailani

Chukua tende 3 ndani ya usiku mwezi 11 Rabī'-ul-Ghaus. Soma suratul fatiha mara moja na suratul Ikhlaas mara moja. Kisha soma maneno yafuatayo mara 11:

يَا شَيْخ عَبْدَ الْقَادِرِ جِيْلَانِيْ شَيْئًا لِلّٰهِ اَلْمَدَد

Soma Salat-'Alan-Nabi mara moja kabla na baada yake kisha puliza juu ya tende moja, rudia kisomo hicho na upulize juu ya tende ya pili na endelea mpaka tende ya tatu. Hakuna ulazima wa tende hizo kuliwa ndani ya usiku huo huo, zinaweza kuliwa hata katika masiku mengine. Utapata nafuu ya magonjwa yote ya tumbo kama vile maumivu ya tumbo, kukosa choo, kujawa na gesi tumboni, vidonda vya tumbo, kutapika na mengineyo.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ط بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ط

Baraka Za Sunnah

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na siasa) sunna za Bwana Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah عزوجل pamoja na niya zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo اِنْ شَآءَ اللّٰه عزوجل tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" اِنْ شَآءَ اللّٰه عزوجل

Kwa ajili ya kusuluhisha nafsi yangu nita fuata Madani In'amaat na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafilah. اِنْ شَآءَ اللّٰه عزوجل

www.dawateislami.net

MC 1286

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262
Web: www.dawateislami.net | E-mail: translation@dawateislami.net